# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY

## ARUSHA TECHNICAL COLLEGE

## KITENGO CHA MAWASILIANO NA MASOKO

*Arusha, 29 Januari, 2026*

## KUSITISHWA KWA SHEREHE ZA WAHITIMU WA MWAKA 2025

Chuo cha Ufundi Arusha (ATC) kinapenda kuwatangazia wahitimu wote mwaka 2025 kuwa sherehe za Wahitimu zilizopangwa kufanyika tarehe 31 Januari, 2026 zimesitishwa.

Uamuzi huu umefikiwa baada ya tathmini kufanyika na kubaini kuwa idadi ya wahitimu waliothibitisha kuhudhuria na kulipia majoho ni ndogo sana **(kati ya wahitimu 908 ni asilimia 7 tu ya wahitimu waliothibitisha kuhudhuria na kulipa fedha za majoho)**, hali inayofanya sherehe hizo kutokuwa na tija kiuchumi na kiutawala kwa wakati huu.

Hata hivyo, kwa wahitimu ambao wameshalipia fedha za majoho, fedha zao zitarudishwa moja kwa moja kwenye akaunti zao. Hivyo basi, kila muhitimu ambae tayari ameshalipia Joho lake anaombwa kutuma taarifa zifuatazo:

1. **Jina kamili**
2. **Jina la Benki**
3. **Nambari ya akaunti**
4. **Stakabadhi ya Malipo (Pay Slip)**

Taarifa tajwa hapo juu zitumwe kwenye Mawasiliano yafuatayo kabla ya tarehe 30 Januari, 2026:

**Barua pepe:cmu@atc.ac.tz au Simu: 0769 00 90 23 (WhatsApp number)**

**Chuo** kinaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza kutokana na mabadiliko haya na kinatoa shukrani kwa ushirikiano na uelewa wenu.

Imetolewa na;

Gasto John Leseiyo

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko**